


KUMILIKI LANGO

LA ADUI BAADA YA KUJARIBIWA

 Sijui kwamba...Unajua, nina wazo dogo, kitu kama, kuwaona watu wamesimama tunaposoma Neno. Hivi hampendi jambo hilo? Tunasimama kuonyesha utii, tunasimama kwa ajili ya taifa letu, kwa nini tusioname kwa ajili ya Neno sasa?

² Wakati tukiwa tumesimama kidogo tu, nilikuwa nikisoma makala fulani, si muda mrefu uliopita, nami nilikuwa nikiwazia jana usiku juu ya wale watu waliomtetea Kristo. Kama hujafanya jambo hilo, je! utalifanya leo?

³ Kulikuwa na mwinjilisti mashuhuri, yapata miaka sabini na tano iliyopita, siwezi tu kukumbuka jina lake. Nafikiri alikuwa Arthur McCoy, naye alikuwa amezunguka nchi nzima. Basi usiku mmoja aliota ndoto ya kwamba alikuwa ameenda Utukufuni. Na alisema alienda mpaka kwenye Lango, naye akasema wasingemruhusu kuingia. Naye akasema alisema, “Mimi ni Arthur McCoy kutoka Marekani. Mimi ni mwinjilisti.”

⁴ Kwa hiyo mlinda lango akaingia, (sasa hii ilikuwa ni ndoto), naye akaingia, kasema, “Siwezi kuona jina lako kabisa.”

Akasema, “Vema, nilikuwa mwinjilisti.”

Akasema, “Bwana, mimi. . .”

⁵ Akasema, “Vema, je! kuna uwezekano kwamba...Kuna kasoro fulani.”

⁶ Akasema, “La, bwana. Ninacho Kitabu hapa. Siwezi kuliona jina lako kabisa.”

Ndipo akasema, “Vema, ninaweza kufanya lolote kuhusu jambo hilo?”

⁷ Akasema, “Unaweza kukata rufani kesi yako kwenye Kiti Cheupe Cha Hukumu.” Mungu, anisaidie. Sitaki kufika pale.

⁸ Akasema, “Vema, kama hilo ndilo tumaini langu pekee, nadhani nitakata rufani tu kesi yangu.”

⁹ Na kisha akasema alifikiri alienda mwendo mrefu sana, na ninii tu. . . Na alipoanza, alisema kulikuwa ni giza, na kukaanza kuwa na nuru zaidi na zaidi, na akasema ilionekana kana kwamba hakuna mahali fulani ambapo Nuru hii ilikoma, bali alikuwa katikati Yake kabisa. Na akasema Yeye alisema, “Ni nani anayekaribia Kiti Changu cha Hukumu?”

¹⁰ Akasema, “Mimi ni Arthur McCoy. Mimi ni mwinjilisti, nimewaingiza watu wengi katika Ufalme”

Akasema, “Je! jina lako halikupatikana kwenye Kitabu?”

“La.”

Kasema, “Basi umekata rufani kwenye Mahakama Yangu?”

“Ndio, Bwana.”

11 “Utaletewa sheria. Nakuhukumu kwa sheria Zangu. Arthur McCoy, hivi ulipata kusema uongo?”

12 Akasema, “Nilifikiri nilikuwa mtu mzuri sana mpaka niliposimama kwenye ile Nuru.” Akasema, “Bali Mbele ya ile Nuru, nilikuwa ni mwenye dhambi.” Sote tutakuwa hivyo. Unaweza ukajisikia uko salama sasa, bali hebu ngojea mpaka utakapofika Pale. Unafikiri inasikikaje hapa wakati Yeye anashusha upako? Jinsi unavyoweza kujisikia duni! Itakuwaje kwenye kile Kiti Cheupe cha Hukumu?

Akasema, “Je! uliwahi kusema uongo?”

13 Akasema, “Nilifikiri nilikuwa mwaminifu, bali baadhi ya vitu vidogovidogo ambavyo nilifikiri vilikuwa ni uongo mdogo usiodhuru, vilikuwa vikubwa na vyeusi Pale.”

Akasema, “Naam, bwana, nimesema uongo.”

Akasema, “Ulishawahi kuiba?”

14 Akasema, “Nilifikiri nilikuwa mwaminifu kwa jambo hilo, wala sijawahi kuiba, bali akasema, Mbele za hiyo Nuru, ni—nilitambua kulikuwa na baadhi ya shughuli nilizofanya, ambazo hazikuwa sawa.”

Akasema, “Ndio, bwana, nimeiba.”

Akasema, “Hukumu Yangu . . .”

15 Na alikuwa tayari yuko karibu kabisa kusikia hukumu yake, “Ondoka uende katika moto wa milele uliowekwa tayari kwa ajili ya ibilisi na malaika zake,” kasema kila mfupa ulikuwa ukitenguka.

16 Akasema, “Nilisikia sauti iliyo tamu kuliko yoyote niliyowahi kusikia maishani mwangu.” Akasema, “Nilipogeuka kuangalia, niliona uso mpole sana niliowahi kuona; mpole kuliko uso wa mama, sauti ya upole zaidi kuliko ya mama yangu alivyowahi kuniita.” Kasema, “Niliangalia pande zote. Nikasikia sauti, ikisema, ‘Baba, hiyo ni kweli, yeye kweli alisema uongo wala hakuwa mkweli kabisa. Lakini, huko chini duniani yeye alinitetea,’ kasema, ‘sasa nitasimama mahali pake.’”

17 Hivyo ndivyo ninavyotaka itendeke Kule. Ninataka kumtetea sasa, ili kwamba, wakati ule utakapofika, Yeye alisimama mahali pang'u.

18 Hebu na tusome kutoka Mwanzo 22; vifungu vya 15, 16, 17, na 18.

Malaika wa BWANA akamwita Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni,

Akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu, asema BWANA, kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee,

Katika kubariki nitakubariki, . . . katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki lango la adui zao;

Na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umetii sauti yangu.

Na tuombe.

¹⁹ Baba wa Mbinguni, chukua fungu hili la maneno sasa, Bwana, na utuhudumie. Jalia Roho Mtakatifu ayachukue Maneno haya, Bwana, moja kwa moja kwenye kila moyo. Hilo lingetimiza matarajio yetu alasiri ya leo, kwa kuwa ni makubwa, Bwana. Nawe ulitwambia kuomba mambo mengi, kusudi furaha yetu itimilike. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

²⁰ Kama ningeita hili fungu la kuhubiria, kwa dakika chache. Sauti yangu ni dhaifu, kwa hiyo hiyo ndiyo sababu inanibidi kusimama karibu na maikrofoni. Ninajua kuna kurudishwa mwangwi, bali na tuvumilie hilo kidogo. Ninataka kuliita: *Kumiliki Lango la Adui Baada ya Kujaribiwa.*

²¹ Picha yetu inaanzia kwenye moja ya matukio ya ajabu sana kwa Ibrahimu. Mnajua ya kwamba Ibrahimu ni baba wa waaminifu. Na ahadi ilitolewa kwa Ibrahimu. Na ni kwa kuwa warithi tu pamoja naye, kwa njia ya Kristo, ndiyo njia pekee tunayopokea ile ahadi, ni kupitia kwa Ibrahimu. Sasa, Ibrahimu alikuwa tu mtu wa kawaida, bali aliitwa na Mungu naye alikuwa mwaminifu kwa wito huo. Wakati Mungu aliposema naye, Ibrahimu hata wakati mmoja hakutilia shaka sauti hiyo hata. Yeye alidumu moja kwa moja nayo. Haidhuru shida ilikuwa ni nini, yeye alidumu moja kwa moja nayo.

²² Na ndipo akaahidiwa mwana. Naye alingojea miaka ishirini na mitano kumpokea huyo mwana, akiita kila kitu kilichokuwa kinyume chake kana kwamba hakikuwa. Na ndipo, na katika mwana huyu, familia zote za duniani zitabarikiwa. Na huyo mzee wetu alikuwa mwaminifu kwa wito wake na Neno lililoahidiwa.

²³ Yeye alikuwa ni mfano kwa yale tunayopaswa kuwa. Sasa sisi, tukiwa wafu katika Kristo, ni Mzao wa Ibrahimu.

²⁴ Sasa, kulikuwa na uzao wa aina mbili wa Ibrahimu. Mmoja wa huo alikuwa ni uzao wa kawaida; huo mwingine ulikuwa Uzao wa kiroho. Mmoja wa huo ulikuwa ni wa kawaida, kwa mwili wake; huo mwingine alikuwa ni Mzao wa imani yake, ile imani, kusudi sisi pia tuwe Uzao wa Ibrahimu kwa Neno lililoahidiwa.

25 Na sasa baada ya yeye kujaribiwa kwa kipindi kirefu cha miaka ishirini na tano, na, badala ya kuwa mnyonge zaidi, alizidi kupata nguvu. Unaona, kama halikutukia mwaka wa kwanza, mwaka ujao lingekuwa ni mwujiza mkubwa zaidi, kwa sababu ilikuwa na umri wa miaka miwili. Naye aliilundika miaka hiyo, wakati akiendelea kuzeeka, na mwili wake ukafa. Tumbo la uzazi la Sara, tumbo la uzazi, ama (likawa) lilikuwa tasa. Na kwa hiyo nguvu zake zilikuwa zimekwisha, na kulikuwa na... Haiwezekani kabisa.

26 Je! uliwahi kuwazia yale Mungu aliyofanya pale? Ona, Yeye hakufanya tumbo lake la uzazi kupata uwezo wa kuzaa kamwe. Kwa kuwa, kumbuka, kama angefanya jambo hilo, basi kumbuka kama angefanya hivyo...hawakuwa na hizi chupa za afya na za usafi, siku hizo, kumnyonyesha mtoto mchanga, maziwa kutoka kwa ng'ombe. Unaona? Pia ilimbidi yeye pia... Vena zake za maziwa zilikuwa zimekauka. Kwa hiyo Yeye—Yeye asingeweza kupata... Ilibidi kuwe na jambo fulani litukie.

27 Halafu, mwangalie mwanamke, mwenye umri wa miaka mia moja, kuingia katika utungu wa kuzaa. Moyo wake usingalistahimili jambo hilo. Ni vigumu sasa kwa mwanamke, mwenye umri wa miaka arobaini, kustahimili jambo hilo. Moyo wake usingaliweza kustahimili jambo hilo. Kwa hiyo unajua alilofanya? Kama utaangalia...

28 Sasa ninajua wengi huenda wasikubaliane. Kama hili ni sawa kufanya tamshi hili? Unaona, mimi...Ingekuwa tu ni mawazo yangu mwenyewe.

29 Unaona, Biblia ni Kitabu cha mbinguni. Kimeandikwa hivi kwamba Kimefichwa kwa seminari, mwanatheolojia. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Yesu alimshukuru Mungu. Yeye alisema, "Ninakushukuru, Baba, Wewe ume-yaficha Hayo kwa wenye hekima na wenye elimu, na kulifunua kwa watoto wachanga wanaoweza kujifunza." Ni kitabu cha mapenzi. Upendo wa Mungu unapoingia moyoni, ndipo unampenda Mungu, ndipo anajifunua Mwenyewe, Biblia inavyomaanisha. Fasiri ya Biblia ni Mungu Mwenyewe akifasiri ahadi Zake. Lakini, Biblia, imeandikwa katikati ya mstari.

30 Sasa, kama vile mke wangu, loo, ndiye mwanamke aliye mzuri sana ulimwenguni mwote, nami kwa kweli ninampenda. Yeye ananipenda. Kwa hiyo ninapokuwa nimesafiri, ataniandikia barua, aseme, "Mpenzi Bill, usiku wa leo ndio kwanza niwaweke watoto kitandani kulala. Leo nimefua, na yote aliyofanya, na kadhalika." Sasa yeye anasema hayo katika barua. Lakini, unaona, ninampenda sana, na tuko zaidi sana kama mtu mmoja, mpaka ni—ninaweza kusoma katikati ya mistari. Ninajua yale anayotaka kusema, unaona, kama ataniambia jambo hilo ama la, unaona. Na—najua yale

anayomaanisha, kwa maana ni upendo wangu kwake, na ufahamu wangu.

³¹ Vema, hivyo ndivyo Biblia ilivyoandikwa. Unaona? U—usomi utakosa hilo moja kwa moja; hawataifahamu kamwe. Unaona, inakupasa ulipende Neno, Yeye, “kumjua Yeye.” Unaona?

³² Sasa, sasa hapa ndani, angalia yale aliyofanya. Sasa Ibrahimu na Sara wote wawili walikuwa wazee, “wazee sana,” ilisema Biblia. Sasa haikuwa tu ni kwa sababu ati watu waliishi kwa muda mrefu zaidi kule. Biblia ilisema ya kwamba “Walikuwa wamezeeka sana.”

³³ Sasa angalia, mara baada ya malaika huyu kutokea, ambaye tumekuwa tukinena habari zake; ambaye alikuwa ni Elohimu, Mungu. Naye alisema, alimwambia Ibrahimu, “Nitakuzuru wakati uu huu mwakani.” Sasa angalia maishani mwao, wao walikuwa ni mfano wa Kanisa, maishani mwao mwote.

³⁴ Sasa angalia. Hivi ndivyo ilivyotukia. Sasa, Yeye si kwamba alimwongezea nguvu Sara, na kumwongezea nguvu Ibrahimu. Aliwageuza wakawa kijana mwanamume na msichana. Sasa huenda jambo hilo likaonekana ni la kushangaza, lakini sasa angalia hilo Neno lengine linalofuatana nalo, na uliweke pamoja. Neno limevuviwa, nawe huna budi kuvuviwa pamoja na Neno. Sasa, kumbuka, mara baada ya jambo hilo, mara baada ya kutokea kwa Malaika huyu. . .

³⁵ Ninaweza tu kuona jambo hilo, hizo nywele zenye mvi za Sara, maskini bibi kizee akiwa na shali mabegani mwake, na kofia yenye mavumbi, ameshika fimbo, akitembea. “Mimi, eti nipate raha na bwana wangu, naye ni mzee, pia?” Unaona? Na huyu hapa Ibrahimu, ndevu ni ndefu hivi, ameshika fimbo, kwa kuwa alikuwa, mzee sana.

³⁶ Pia ninaona, kesho yake asubuhi, mabega yake yalianza kunyoka, na kibyongo kikatoka mgongoni mwake. Nywele za mkewe zikaanza kubadilika. Wakarudi wakawa kijana mwanamume na msichana. Ikionyesha tu yale atakayoufanyia Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, unaona, wakati “tutakapobadilishwa mara moja, katika kufumba na kufumbua, na kunyakuliwa pamoja.”

³⁷ Angalia kilichotukia. Sasa hebu niwathibitishie jambo hili. Sasa walisafiri kwa miguu kutoka mahali hapo walipokuwa, huko Gomora; na wakaenda mpaka Gerari, wakashuka mpaka nchi ya Wafilisti. Je! ulijua? Hebu paangalieni kwenye ramani, kwamba pana umbali gani. Ni safari ndefu sana kwa mume na mke wakongwe wa umri huo.

³⁸ Halafu tena, mbali na hayo, katika—katika nchi ya Wafilisti kule, kulikuwa na mfalme kijana kwa jina la Amaleki, naye alikuwa akitafuta mke. Naye alikuwa na wasichana hao wote warembo wa Kifilisti, bali wakati alipomwona bibi kizee huyu, alisema, “Yeye ana sura nzuri sana,” naye akampenda na alitaka

kumwoa. Hiyo ni kweli. A-ha. Unaona, alikuwa mzuri wa uso. Unaona?

³⁹ Alikuwa amegeuka akawa kijana mwanamke. Angalia, ilitibi abadilike awe hivyo, apate kumzaa huyo mtoto. Mungu alimfaya kuwa kiumbe kipya. Naye alipaswa kuwa ninii, kumlea mtoto huyu. Na kumbukeni, Ibrahimu, “mwili wake ukiwa kama mfu,” na Sara alikufa wakati Ibrahimu alipokuwa... Isaka alipokuwa na umri wa miaka arobaini na mitano, ninaamini, wakati Sara alipokufa. Na Ibrahimu akaoa mwanamke mwingine kupata wana saba mbali na binti kadhaa, baada ya hapo. Ha-ha! Amina.

⁴⁰ Unaona, soma katikati ya mistari. Ni mfano. Inaonyesha hapo kile atakachowafanyia watoto wote wa Ibrahimu. Vile vile tunapokaribia jambo hilo kabisa sasa, kwa hiyo mabega yetu yaliyoinama na kila kitu hayaleti tofauti yoyote, wapendwa. Na nywele zetu zenye mvi na chochote kile, haijalishi sasa. Hatuungalii nyuma. Hebu na tuangalie mbele kwa yale tunayokwenda.

⁴¹ Pia kumbukeni, ishara hii tunayoiona, ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu na Sara wake waliyoiona, kabla ya kuja kwa yule mwana aliyeahidiwa. Tunaamini tuko kwenye saa hiyo.

⁴² Yule mzee wetu, baada ya kuzaliwa kwa mvulana huyu. Ungeweza kuwazia Isaka, yapata umri wa miaka kumi na miwili; maskini mvulana mdogo wa kupendeza mwenye nywele za kipilipili, macho madogo ya hudhurungi? Ningeweza kuwazia jinsi mama huyo alivyojisikia; kijana mwanamke mrembo, na kwa hiyo, na baba yake. Na siku moja, Mungu akasema, sasa, kwa mfano; tuko mbali sana, na ile saa ambapo hilo litakapotukia. “Nimekufanya wewe baba wa mataifa, kupitia kwa mvulana huyu, bali ninataka umchukue mvulana huyu mpaka juu ya mlima nitakaokuonyesha, nami ninataka umchinje kule juu, awe dhabihu.” Ungeweza kuwazia jambo hilo?

⁴³ Sasa hujapata kuambiwa kwenda kwenye jaribio kama hilo. Yeye hafanyi hivyo wakati huu. Hiyo ilikuwa ni mfano, vivuli.

⁴⁴ Je! Ibrahimu alihofu? La, bwana. Ibrahimu alisema jambo hili, “Mimi nimeshawishika kabisa ya kwamba Yeye anaweza kumfufua kutoka katika wafu, kwa kuwa nilimpokea kama mtu aliyetoka kwa wafu. Na kama hiyo amri ya Mungu iliniambia nifanye jambo hili, nami nimedumu mwaminifu kwalo, na likawa na matokeo mazuri, kunipa mimi huyo mwana; Mungu anaweza kumfufua kutoka katika wafu; ambako kutoka huko nilimpokea, kama mfano.”

⁴⁵ Loo, jamani, mpendwa! Kama Mungu aliwapa ninyi Wapentekoste Roho Mtakatifu, mkinena kwa lugha, ni zaidi sana vipi mnavyopaswa kuamini nguvu Zake za kuponya, na wema Wake na rehema! Kama alifanya jambo hilo,

dhidi ya wanatheolojia wote nchini! Walisema jambo hilo lisingewezekana, bali Mungu alilifanya kwa maana aliliahidi. Basi simama na Bunduki yako, Neno lako, Upanga wako, liamini Neno la Mungu. Mungu alisema hivyo, na hilo latosha!

⁴⁶ Angalia, sasa, ilimchukua safari ya siku tatu kutoka hapo, akiwa na nyumbu. Sasa ninaweza kutembea, wakati nilipokuwa kwenye doria, nilitembea maili thelathini kila siku, katika nyika; nasi tuna miguu ya petroli, kitu kama hicho. Lakini watu hao, njia pekee ya usafiri wao, ilikuwa ni aidha kupanda punda ama—ama kutembea kwa miguu. Naye alisafari safari ya muda wa siku tatu kutoka mahali alipokuwa, ndipo akayainua macho yake, huko nyikani, na kuona ule mlima ukiwa mbali.

⁴⁷ Akamchukua Isaka na akaifunga mikono yake. Ambapo, sote tunajua, katika Mwanzo 22 hapo, ni mfano wa Kristo. Akamwongoza juu kupanda mlimani, amefungwa, kama vile Yesu alivyoongozwa juu mlimani, Mlima wa Kalvari; mfano wa Mungu akimtoa Mwanawe, bila shaka.

⁴⁸ Lakini walipofika kule juu, naye alikuwa mtiifu, Isaka alianza kushuku. Akasema, “Baba, hizi hapa kuni, hii hapa madhabahu, huu hapa moto, bali dhabihu iko wapi?”

⁴⁹ Naye Ibrahimu, akijua niani mwake, hata hivyo Neno la Mungu limesimama pale, akasema, “Mwanangu, Mungu anaweza kujipatia dhabihu kwa ajili Yake Mwenyewe.” Akapaita mahali pale, “Yehova-yire.”

⁵⁰ Na alipomfunga mwanawe, huyo mwana alikuwa mtiifu hata mauti; alimlaza juu ya madhabahu, akachomoa kisu kutoka katika ala, na akaanza kuutoa uhai wa mwanawe mwenyewe. Na, alipofanya jambo hilo, kitu Fulani kiliushika mkono wake, na kusema, “Ibrahimu, ondoa mkono wako.”

⁵¹ Na wakati uo huo, kondoo mume akalia, nyuma yake, amenaswa pembe zake huko porini.

⁵² Je! ulipata kuwazia, je! kondoo mume huyo alitoka wapi? Kumbuka, nchi hiyo imejaa simba na mbwa mwitu na mbweha, na wanyama wanaowala kondoo. Na alikuwa umbali gani kutoka kwa watu? Na, tena, huko juu kwenye kilele cha mlima, ambako hakuna maji. Naye alikuwa ameokota mawe, hapo na pale pote, kujenga madhabahu hiyo. Je, kondoo huyo mume alitoka wapi? Unaona?

⁵³ Lakini halikuwa ni ono. Yeye alimchinja huyo kondoo mume; alikuwa na damu. Yeye alisema nini? “Mungu anaweza kujipatia sadaka kwa ajili Yake Mwenyewe.”

⁵⁴ *Wewe* utatokaje kwenye kiti hicho? Je! *huyo* mtoto mwenye degedege ataponaje, ama *wewe* kutoka katika kiti hicho, *wewe* hapo ulipo, *wewe* mwenye ugonjwa wa moyo? Shida yoyote ile, “Mungu aweza kujipatia Mwenyewe.”

55 Ibrahimu aliamini jambo hilo. Huyu mzee wetu alidumu mwaminifu kwa ile ahadi. Naye alitoa ahadi, ya kwamba, “Uzao wako! Kwa sababu umeamini Neno Langu, na haidhuru hali ya mambo ikoje, uzao wako utamiliki lango la adui zake.”

56 Kwa nini? Kila adui aliyekuja, kama mfano, dhidi ya Ibrahimu, Ibra-...Adui ya, “Mke ni mzee mno. Mimi ni mzee mno. Yote *haya*, na chochote kile.” Yeye bado alidumu mwaminifu kwa ahadi ile.

57 Sasa, mwanadamu aliye na imani hiyo, angali atachukua Neno la Mungu haidhuru hali ya mambo ikoje. Sasa, kama huwezi kufanya jambo hilo, basi wewe si uzao wa Ibrahimu. Hiyo ndiyo imani aliyokuwa nayo Ibrahimu, Uzao wake.

58 Ahadi ya Ibrahimu ilikuwa ya kwamba “Uzao” wake, sasa Uzao wake wa kifalme, pia, kama nilivyowaambia muda mfupi uliopita. Na muhuri huu aliompaa Ibrahimu, ulikuwa ni muhuri wa ahadi. Na Uzao wa kifalme, kulingana na Waefeso 4:30, ni “kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu,” baada ya wao kustahimili jaribio. Hebu jaribu kuwazia jambo hilo.

59 Wengi wanafikiri wana Roho Mtakatifu. Wengi wanadai wana Roho Mtakatifu. Wengi wanaweza kuonyesha shuhuda nyingi na ishara zake. Lakini, hata hivyo, kama hawezi kukaa na Neno hili, si Roho Mtakatifu. Unaona?

60 Unaamini kila Neno, ndipo unatiwa muhuri baada ya jaribio. Tunapoamini kila ahadi katika Neno, basi tunatiwa muhuri na Roho, kuthibitisha ile ahadi. Hivyo ndivyo, ndivyo Ibrahimu, jinsi alivyofanya jambo hilo. Ndipo, na hapo ndipo tu, tunapokuwa na haki ya kumiliki lango la adui zetu. Huwezi kufanya jambo hilo mpaka kwanza uwe Uzao huo. Kumbuka, katika Biblia...

61 Nilizungumza juu ya jambo hilo, kule Houston ama mahali fulani, hivi...ama, ninamaanisha, Dallas. *Ile Ishara*.

62 Unaona, M—Myahudi angeweza kuonyesha, huko Israeli, ya kwamba yeye alikuwa ni Myahudi kwa tohara. Lakini Mungu alisema, “Nitakapoiona damu! Na hiyo damu itakuwa ni ishara kwenu.”

63 Ule uhai uliokuwa katika damu usingeweza kumrudia mwabuduo, kwa sababu, vema, ulikuwa ni uhai wa mnyama, ulikuwa ni kivuli tu kilichoelekea kwenye Uhai halisi. Halafu, ile kemia, ile damu yenyewe, ilipaswa kuonyesha rangi nyekundu juu ya mlango na miimo ya mlango.

64 Ikiwa imepakwa kwa hisopo, ambalo ni gugu la kawaida, ikionyesha ya kwamba haikubidi kuwa na imani kubwa sana. Inakubidi tu uwe na ile ile, imani uliyo nayo, kama ile uliyo nayo ya kuwasha moto gari lako, kuja kanisani. Unaona? Watu wengi sana wanafikiri wanapaswa wao kuwa kitu fulani...Lakini, la, la, hilo ni kosa. Ni imani ya kawaida tu ndiyo tu unayopaswa

kutumia kupaka nayo hiyo Damu. Kusikia Neno, na kuliadini Neno, itumie, hivyo tu. Okota magugu popote pale Palestina, yalikuwa ni ya hisopo, gugu dogo tu lililoota kwenye nyufa za kuta, hapa na pale, wakaichovya katika damu yao na kuipaka kwenye miimo na vizingiti vya milango.

⁶⁵ Na, kumbukeni, sijali walikuwa katika agano jinsi gani, ni kiasi gani Myahudi angeweza kuonyesha ya kwamba alikuwa ametahiriwa, jinsi mtu huyo alivyokuwa mzuri, agano lote lilibatilishwa isipokuwa ile—ile ishara iwe imewekwa. “Nitakapoiona hiyo damu,” peke yake.

⁶⁶ Sasa, Damu sasa, ile Ishara, si ile yenyewe, Damu yenyewe ya Kristo, maana ilimwagwa maelfu ya miaka iliyopita.

⁶⁷ Lakini, unaona, pale ambapo ninii. . . ilibidi kuwe na kemia pale, ule uhai uliokuwa katika huyo mnyama usingeweza kuja juu ya mwanadamu, kwa sababu uhai wa mnyama hauna nafsi. Wanyama hawapambanui jema na baya. Mwanadamu ndiye aliye na nafsi.

⁶⁸ Sasa, lakini wakati Yesu, Mwana wa Mungu, aliyezaliwa na bikira, alipoimwaga Damu Yake, ule Uhai uliokuwa katika hiyo Damu ulikuwa ni Mungu Mwenyewe. Biblia ilisema, “Tunaokolewa na Uhai, Damu ya Mungu.” Si damu ya Myahudi, si damu ya Mmataifa; bali ni Uhai wa Mungu. Mungu aliiumba hii seli ya Damu, iliyojaliwa na bikira. Yeye hakumjua mwanamume kamwe, wala yeye. . . wala yai halikutoka kwake.

⁶⁹ Ninajua wengi wenu ninyi watu mnataka kuamini yai hilo lilitoka kwake. Hilo yai haliwezi kushuka hapo bila ya msisimko, Mungu angefanya kitu gani hapo? Unaona?

⁷⁰ Yeye aliumba yai na seli ya Damu, na hiyo ilikuwa ndiyo maskani ya Mungu, takatifu. “Sitamwacha Mtakatifu Wangu kuona uharibifu.” Unaona mahali hilo yai lilipotoka? “Wala sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu.” Mwili Wake ulikuwa mtakatifu! Loo, jamani! Huninii, huwezi kuamini jambo hilo, unaweza je kujiita Mkristo?

⁷¹ “Tunaokolewa kwa Damu ya Mungu.” Hapo ndipo imani Yangu ilipo. Si kutembea kwenda huko nje katika damu ya nabii, si kutoka na kwenda huko nje katika damu ya mtu fulani wa kawaida, ama mwalimu fulani, ama mwanatheolojia. Tunatembea pale katika Damu ya Mungu. Mungu alisema jambo hilo. Yeye alifanyika mwanadamu. Alibadilisha sura Yake. Alitandaza hema Yake hapa, pamoja na sisi, na akawa mmoja wetu. Yeye ni Mkombozi wa Jamaa yetu aliye karibu. Ilibidi afanyike wa jamaa yetu kwetu, kwa kuwa hiyo ilikuwa ndiyo sheria. Mungu alifanyika mtu na akakaa kwetu.

⁷² Angalia jinsi ambavyo, katika kufanya jambo hili, Yeye akitoka Kwake, alikuwa ni Mungu, yule Roho, na huyo Roho anakuja juu ya mwaminio. Kwa hiyo Uhai uliokuwa ndani ya Dhahihu yetu, tunatambulishwa na Uhai uo huo.

⁷³ Basi wanawezaje kuona Uhai wa Mungu ukitenda kazi miongoni mwa watu, na kuuita kitu kichafu, wakati huo ndio utambulisho wetu wa Dhabihu yetu? “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya.” Uhai Wake ukirudi juu ya dhabi- . . . kutoka kwa Dhabihu, tunapoweka mikono yetu juu Yake na kujitambulisha wenyewe kuwa wafu kwa mawazo yetu. Basi tunawezaje kuacha madhehebu yatusukume kutuingiza katika kanuni za imani na kadhalika, na kusema tuamini jambo Hilo? Tumekufa kwa mambo hayo.

⁷⁴ Paulo alisema, “Hakuna yoyote ya mambo haya yanayonisumbua,” kwa kuwa yeye alikuwa amefungwa kwenye yakini, Kristo. Na kila fanikio la kweli hufungwa kwenye yakini, na yakini yangu ni Neno. Na kila mtu mwingine amefungwa kwenye yakini, ambaye—ambaye amezaliwa kwa kweli na Roho, yakini yao ni Neno la Mungu. Nimefungwa Kwake. Niliweka mikono yangu juu Yake. Na ilipachukua mahali pangu, nami nimejitambulisha pamoja Naye. Tulijua ya kwamba Yeye aliahidi kujitambulisha pamoja na sisi. Hilo linaleta imani halisi; si imani yako mwenyewe, bali imani Yake; kitu ambacho hukidhibiti. Yeye hukidhibiti. Sasa angalia. Ndipo, na ndipo tu, ambapo ninii . . . ndipo ile ahadi imetolewa kwako.

⁷⁵ Haidhuru ulijiunga na makanisa mangapi, umebatizwa mara ngapi; kifudufudi, kichalichali, vyovyote unavyotaka. Mpaka muhuri huo utakapowekwa juu yako, basi huna haki ya kujiita mwenyewe kwamba umeunganishwa na Dhabihu yako.

⁷⁶ Na Muhuri wa Mungu ni nini? Waefeso 4:30, inasema, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mmetiwa muhuri hata Siku ya ukombozi wenu.” Si kutoka ufufuo mmoja mpaka mwingine, bali mmetiwa muhuri Milele mpaka Siku utakayokombolewa urudishwe.

⁷⁷ Na, kumbukeni, kama kamwe hujapata kuwa katika mawazo ya Mungu, kamwe hutapata kuwa pamoja na Mungu. Ni wangapi wanajua ya kwamba Yeye alikuwa mkombozi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, basi, chochote kilichokombolewa hakina budi kurudi hadi mahali kilipoangukia. Kwa hiyo kama Yeye alikuja kutukomboza, tungewezaje sisi, ambao wakati mmoja hatukuhitaji kukombolewa, na sote “tulizaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja ulimwenguni tukisema uongo”? Inaonyesha ya kwamba Mkristo halisi ni sifa za mawazo ya Mungu, kabla hapajakuwapo na ulimwengu, wala nyota, wala hewa, wala chochote kile. Ni Sifa ya Milele, na Yeye alikuja kutukomboza turudi. Ni wazo la Mungu, lililotamkwa likawa neno, likadhihirishwa na kuninii . . . kurudishwa kwenye wazo Lake.

⁷⁸ Mkombozi aliye Jamaa yetu! Hiyo ndiyo sababu ilimbidi Mungu Mwenyewe kufanyika mmoja wetu, apate kukomboza.

Hakuna kitu kingine kingaliweza kufanya jambo hilo. Malaika asingeweza kufanya hivyo, hakuna kitu kingine. Ilimbidi kushuka, apate kujaribiwa jinsi tunavyojaribiwa, apate kutukomboa.

⁷⁹ Angalia sasa uzao wa kawaida wa Ibrahimu. Hebu na tuangalie baadhi ya huo uzao wa kawaida, na tuone kama Mungu alitimiza Neno Lake kwa uzao wa maumbile ya kawaida, ambao ulikuwa ni Isaka. Hebu na tuangalie baadhi ya uzao wa kawaida ulioamini ahadi yote ya Mungu wala haukuwa na swali. Sasa kumbuka, kulikuwa na maelfu kumi mara elfu mara maelfu ambao walitahiriwa na chochote kile, na hata hivyo hawakuwa Uzao wa Ibrahimu. Hakika, “Hao walio Wayahudi kwa nje si Wayahudi; ni wale walio Wayahudi kwa ndani.” Wao, wengi wao, walishindwa, walishindwa vibaya.

⁸⁰ Angalia, kule nyikani, wao walisema, “Sisi. . .” Ile siku ya Pasaka, ama kwenye kule kunywa pale penye ile chemchemi, Yohana Mtakatifu 6. Wote walikuwa wakifurahi.

⁸¹ Yesu alisema, “Mimi Ndimi ule Mwamba uliokuwa nyikani. Mimi ni Mkate uliotoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni, mtu akiweza kuula wala asife.”

⁸² Wao walisema, “Baba zetu walikula mana jangwani, kwa muda wa miaka arobaini.”

Yeye akasema, “Na wote, kila mmoja wao, amekufa.”

⁸³ *Kufa*, chukua neno hilo ulifuatilie, uone lina maana gani, “Kutengwa milele.” Hata hivyo, walikuwa ni uzao wa Ibrahimu. *Mauti* maana yake ni “kutengwa, kuangamizwa, kuharibiwa kabisa, kuangamizwa.” Yesu alisema walikuwa wamekufa, kila mmoja wao, hata hivyo walikuwa Wayahudi waliotahiriwa.

⁸⁴ Unaona, maskini jamaa hao, kwa sababu tu sisi ni Methodist, Baptisti, Presbiteri, tuna kukiri kudogo, na vitu kama hivyo; ibilisi anaamini jinsi vilevile sisi nasi tunavyoamini.

⁸⁵ Lakini huna budi kutambulishwa Nalo. Mungu hana budi kushuhudia Hilo, kwa kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Hakuna swali la Neno!

⁸⁶ Kama ukisema, “Vema, sasa, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine,” kuna kasoro fulani.

⁸⁷ Vipi kama mtu alikuja mbio, nawe ulimwambia nuru ilikuwa ikiangaza, naye akakimbilia kwenye chumba cha chini ya nyumba, akasema, “Ninakataa kabisa jambo hilo. Ninalikataa kabisa. Hakuna kitu kama nuru. Siamini kitu hicho”? Mtu huyo angekuwa na kasoro. Angekuwa amechanganyikiwa kiakili. Kama anakataa miali yake yenye joto na uwezo wake wa kutoa uhai, ana kasoro fulani, kiakili.

⁸⁸ Na wakati mtu anapoliona Neno la Mungu, likifanywa dhahiri mbele zake, na kuwekwa bayana, na halafu anafunga na kushusha mapazia yake ya kimadhehebu, mtu huyo ana kasoro

fulani, kiroho. Ana kasoro fulani. Kuna kasoro fulani ya kiroho. Yeye hawezi kulipokea kabisa. “Kipofu, wala hajui,” akielekea kwenye ile Hukumu, na Mungu ndiye atakuwa hakimu.

⁸⁹ Angalia wakati wao—walipofanya jambo hili, na uzao huu sasa ambao uliliamini, angalia jambo lililotukia. Hebu na tuangalie baadhi yao sasa, Uzao wa Ibrahimu.

⁹⁰ Hebu tuwachukue wana wa Kiebrania, maana wao walisimama kwa uaminifu wala wasingevumilia ibada za sanamu. Walikataa kusujudia sanamu ambayo mfalme wa nchi alikuwa ameitengeneza. Ilitengenezwa kwa mfano wa mtu mtakatifu, pia, sanamu ya Danieli.

⁹¹ Inaonyesha ya kwamba jamii ya Mataifa iliingizwa chini ya upande wa uongo, wa kuabudu sanamu ya mtu mtakatifu. Jamii hiyo inaishia vivyo hivyo, wakati watu watakapolazimishwa kuabudu sanamu za watu. Ilitokana na ufunuo, wa Danieli akiwa na uwezo wa kufasiri Neno, ambalo liliandikwa kwa maandiko ya mkono kwenye ukuta. Hivyo ndivyo ilivyoingia, na hivyo ndivyo itakavyoishia, vivyo hivyo, kwa sanamu ya Mataifa.

⁹² Angalia, walikataa kufanya jambo hilo. Nao walifanya nini? Walikuwa ni uzao wa Ibrahimu wakiwa waaminifu kwa Neno, nao wakaumiliki mlango wa adui, wa moto. Waliumiliki. Vema, Neno la Mungu ni kweli.

⁹³ Danieli, alijaribiwa kwa kuabudu Mungu mmoja wa kweli. Yeye alijaribiwa kwa jambo hilo. Na katika wakati wa kujaribiwa, yeye alistahimili jaribio hilo. Na Mungu alifanya nini, baada ya mambo kuonekana kana kwamba yamemwendea mrama, kama vile ambavyo tungenesema? Nao hawakujua la kufanya. Walikuwa wakitaka kwenda kumlisha kwa simba. Bali Danieli alidumu mwaminifu kwa hilo jaribio, ya kwamba kuna Mungu mmoja wa kweli, naye akamiliki lango la adui yake. Mungu alikuwa amekifunga kinywa cha simba.

⁹⁴ Musa alidumu mwaminifu kwa neno lililoahidiwa, mbele ya wale waigaji wa uongo, Yambre na Yane, kwenye lile jaribio. Angalia, Mungu alikuwa amekutana naye, akiwa na ishara za kimbinguni, akamwambia aende akafanye mambo haya, akaonyeshe ishara hizi, na kila ishara ingekuwa na sauti. Musa alishuka akaenda moja kwa moja, akiwa mnyofu tu kadiri alivyojua. Akatupa hizo fimbo chini, nayo ikageuka kuwa nyoka. Unajua yaliyotukia? Hawa hapa waigaji wakaja na kufanya jambo lile lile.

⁹⁵ Sasa, Musa hakutupa mikono yake juu, aseme, “Vema, nadhani hayo yote ni uongo mtupu.” Alikaa pale na kumngojea Mungu. Alidumu mwaminifu. Haidhuru kulikuwako na waigaji wangapi, yeye alidumu kuwa mwaminifu. Na wakati alipodumu mwaminifu kwa agizo lake, kuwatoa hao watu kutoka mahali hapo. Wakati lango la maji lilipomzuia, Mungu alimjalialia

kulimiliki, Naye akalifungua lango hilo kwa Nguzo ya Moto iliyokuwa ikimwongoza. Akawachukua watu akawapeleka hadi nchi ya ahadi.

⁹⁶ Yoshua, kiongozi mwingine mkuu. Ni wawili tu kati ya... walioingia kwenye nchi ya ahadi, Yoshua na Kalebu. Walifika mahali panapoitwa Kadesh, ambapo palikuwa ndipo kituo kikuu cha dunia wakati huo, kiasi kwamba palikuwa ndipo kiti cha hukumu. Na, loo, waliwatuma wapelelezi kumi na wawili kuiangalia nchi, na kumi na wawili wa hao wakarudi.

⁹⁷ Kumi wa hao walisema, "Loo, ni kazi kubwa sana. Tusingeweza kufanya jambo hilo kabisa. Vema, hao watu, tunaonekana kama panzi tukiwa karibu nao."

⁹⁸ Lakini Yoshua alifanya nini? Aliwatuliza watu. Akasema, "Ngojeni kidogo. Tuna uwezo hata na zaidi kuiteka, haidhuru sisi ni wadogo jinsi gani, ama tuko katika uchache kiasi gani." Yeye alikuwa akifanya nini? Alikwa akidumu mkweli kwa ile ahadi, "Nawapa nchi hii," bali mtapigania kila inchi ya ardhi yake.

⁹⁹ Je! unaamini jambo hilo, mama? Mungu amekupa uponyaji wako, bali utapigania wote mzima. "Kila mahali ambapo unyayo wa miguu yako unapokanyaga, ninakupa hapo upamiliki." *Nyayo za miguu* maana yake ni "kumiliki." Ni pako pote, kila ahadi ni yako, bali utapigania kila inchi ya njia yote kuingia sasa.

¹⁰⁰ Sasa, Yoshua alijua yale Mungu aliyosema. Yeye alikuwa ni uzao wa Ibrahimu. Unaona? Yeye alisema, "Ninaamini jambo hilo, ya kwamba Mungu alitupa nchi hii, nasi tunaweza hata na zaidi kuiteka." Na kwa sababu yeye alistahimili hilo jaribio, dhidi ya kundi lote la Waisraeli, makabila yote na watu wote waliomboleza na kulia. Yoshua akasema, "Tulieni! Mungu alitoa hiyo ahadi."

¹⁰¹ Haidhuru wewe u mkubwa jinsi gani, na upinzani ukoje, na yale daktari aliyosema, Mungu alitoa ahadi. Ni juu ya Mungu kuitimiza.

¹⁰² Yeye alifanya nini? Aliposhuka akafika mtoni Yordani, alimiliki lango hilo. Hivyo ndivyo a—alivyofanya.

¹⁰³ Yeriko, ilifungwa kama kasa kwenye ganda lake. Je! yeye alifanya nini? Alimiliki hilo lango.

¹⁰⁴ Hata siku moja wakati adui yake alipokuwa akijaribu kumkamata, yeye alimiliki lango la adui yake sana hivi kwamba aliamuru jua lisimame kimya. Na jua likamtii, wala halikugeuka kwa muda wa saa ishirini na nne.

¹⁰⁵ Mungu ni mwaminifu kwa ahadi Yake, haidhuru itamlazimu kufanya nini; kufilisi Mbingu kabla hajaliacha Neno Lake lishindwe. Yeye kamwe hajawahi kuweka ahadi ambayo hawezi kuitimiza. "Mimi ni Bwana akuponyaye magonjwa yako yote.

Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Amina. “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

¹⁰⁶ Yoshua aliamini jambo hilo, ingawa ilimbidi Mungu kusimamisha dunia isizunguke. Aliishikilia pale kwa Nguvu fulani nyingine, nguvu Zake Mwenyewe; hivi kwamba dunia haikuzunguka kabisa kwa muda wa saa ishirini na nne, mpaka Yoshua alipojilipiza kisasi juu ya adui zake. Aliyateka hayo malango. Hakika, aliyateka. Mungu ni mkweli daima.

¹⁰⁷ Sasa laiti tungalikuwa na wakati wa kuwafikia mashujaa wengi zaidi, bali nina kama dakika kumi sasa. Angalieni, hawa mashujaa wote wa thamani, vile walivyokuwa, na askari hodari wa imani, wote walikufa kwenye lango la mauti. Wote waliangamia, papo hapo kwenye lango la mauti.

¹⁰⁸ Ndipo moja kwa moja ukaja Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Wote walikuwa uzao wa maumbile ya kawaida, toka Isaka. Lakini hapa ukaja Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, ambao ulikuwa ni Kristo, Uzao wa Ibrahimu wa imani; kile tunachopaswa kuwa, hebu tuone tu kama ndivyo tulivyo ama sivyo. Uzao huo wa kawaida ulikuwa tu ni mfano. Wengine wote walizaliwa kwa uzao wa maumbile ya kawaida, bali Yeye alikuja kwa kuzaliwa na bikira. Unaona, huyo hakuwa ni wa uzao wa Ibrahimu, basi, Myahudi. Alikuwa kwa njia ya uzao wa imani wa ile ahadi. Na, basi, tunapaswa kuwa watoto Wake, kupitia kwa Mtu huyu.

¹⁰⁹ Angalia kile Yeye alichofanya. Wakati alipokuwa duniani, alishinda na kumiliki kila lango alilokuwa nalo adui; huo Uzao wa Kifalme. Yeye aliahidi hilo kwa Neno. Alilishinda. Alishinda lango la magonjwa, kwa ajili yetu. Hilo ndilo Yeye aliokuja kufanya. Yeye, kumbukeni, enyi wagonjwa, Yeye alishinda lango hilo. Haikubidi kulishinda; Yeye alilishinda. Hao watu wengine ilibidi kushinda lango lao wenyewe. Bali haikubidi kushinda; limeshindwa tayari. Yeye alishinda malango ya magonjwa. Naye alifanya nini wakati aliposhinda malango ya magonjwa, akisema ya kwamba angefanya hivyo? “Lolote utakaloomba duniani, na lolote umefunga duniani, Yeye angelilifunga Mbinguni,” linatupa sisi funguo za hilo lango.

¹¹⁰ Alishinda lango la majaribu, kwa Neno. Na funguo hizo zilikuwa, “Mpingeni Shetani, naye atawakimbia.” Yeye alilishinda lote; alishinda kila ugonjwa.

¹¹¹ Alishinda mauti, na alishinda kuzimu. Alishinda mauti na kuzimu. Alishinda yale wengine wasingeweza kushinda, kwa kuwa wao ni wa uzao wa kawaida. Huu ni Uzao wa kiroho. Yeye alishinda lango la kaburi, kisha akafufuka katika siku ya tatu, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu.

¹¹² “Na sasa sisi tu zaidi ya washindi.” Tunaingia moja kwa moja ndani yake, kama urithi, “Zaidi ya washindi.” Sasa tunashughulika na adui aliyeshindwa. Magonjwa

yameshindwa. Mauti imeshindwa. Kuzimu kumeshindwa. Kila kitu kimeshindwa. Loo, jamani! Laiti ningalikuwa mkubwa maradufu ya ukubwa wangu, sasa labda ninajisikia vizuri maradufu. Tunabishana na adui aliyeshindwa.

¹¹³ Si ajabu Paulo aliweza kusema, wakati walipokuwa wakijenga bloku wapate kukata kichwa chake, alisema, “Ee mauti, u wapi uchungu wako? Nionyeshe mahali ambapo unaweza kunifanya nifadhaike na kupiga mayowe. Kaburi, u wapi ushindi wako, na unadhani utanifinyanga huko ng’ambo? Nitakuonyesha lililo wazi kule upande wa pili; nami nimo ndani Yake, Yeye atanifufua katika siku ya mwisho.” Adui aliyeshindwa!

¹¹⁴ Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu! Sasa, uzao wa kawaida usingeweza kuelekeza kidole chake kwenye jambo Hilo. Bali Uzao wa Kifalme unaweza kushinda, tayari umeshinda, kwa kuwa Yeye ametangulia mbele yetu na kushinda kila lango kwa ajili yetu. Yeye sasa, baada ya miaka elfu mbili, Yeye anasimama katikati yetu, yule Mshindi mkuu. Si kwamba tu Yeye alishinda magonjwa...Alishinda magonjwa. Alishinda majaribu. Alishinda kila adui. Alishinda mauti. Alishinda kuzimu. Alishinda kaburi, kisha akafufuka tena. Na miaka elfu mbili baadaye, huyu hapa amesimama miongoni mwetu, alasiri ya leo, akijitambulisha Mwenyewe, yule Mshindi mkuu! Amina.Yeye angali yuko hapa, akiwa hai, akithibitisha ahadi Yake, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu! Loo, jamani! Na adui ataninii. . .

¹¹⁵ “Atashinda malango ya adui yake.” Kwa hao, Uzao, Yeye anasimama hapa akiwa hai kujithibitisha Mwenyewe kwa nani? Hao Uzao uliochaguliwa tangu zamani ambao wanaweza kuliona. Yeye alishinda hilo. Yeye ambaye, baada ya jaribu, la ahadi ya Neno, walitiwa muhuri na Roho Mtakatifu, ndani Mwili wa Kristo, kwao inathibitisha (nini?) kwamba Waebrania 13:8 ni kweli. Wametiwa muhuri wakawekwa ndani na Roho Mtakatifu, yule Roho Mtakatifu ambaye alikuja kwa . . . Ibrahimu alitangulia kumwona; kwa imani aliamini hilo. Na sasa sisi tunampokea, tukiangalia nyuma kwenye ahadi ya yale Yeye aliyosema. Na Yohana 14:12 inathibitishwa katika siku hizi za mwisho, na yule Mshindi aliyefufuka, Mwenyewe.

¹¹⁶ Si mfumo fulani; bali ni Mtu, Kristo, yule Mshindi. Si kanisa langu, si kanisa langu la Kibaptisti, wala lako la Kipresbiteri, Methodist, wala la Wapentekoste, si kwa hayo; bali ni kwa Yesu Kristo. Yeye yu hai leo. Alifufuka juu ya jambo hilo, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu.

¹¹⁷ Na kwa kuwa Yeye yu hai, Yeye alisema sisi nasi pia tunaishi. “Mtu haishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno,” si sehemu ya Neno, “kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” “Mimi Ndimi Ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa,

atakuwa anaishi. Kila aishiye na kuniadini hatakufa kabisa. Je! unayasadiki hayo?” Teki lango la kila adui!

¹¹⁸ Angewezeje kumshinda Bosworth, wakati Mungu... Bosworth alikuwa ndani ya yule Mshindi. Na hiyo ndiyo sababu yeye alisema, “Saa ya furaha sana kuliko zote maishani mwangu ni sasa.” A-ha. Yeye alimjua yule Mshindi Mwenye Nguvu. Yakini yake ilikuwa Kwake. Loo, jamani! Sasa tunaweza kuimba:

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele;
Siku moja Yeye anakuja, Ee siku yenye utukufu!

¹¹⁹ Kwa wale wanaonekana kana kwamba wameshindwa. Eddy Perronet, naamini ilikuwa ni Yeye, asingeweza kuuza nyimbo zake za Kikristo. Hakuna mtu aliyezetaka. Hawakuzithamini hata kidogo. Loo, alishindwa, na ni mwamini! Siku moja, Roho Mtakatifu alishuka juu yake. Lango la adui wake, ambaye asingepokea vitabu vyake! Roho alimgusa, ndipo akanyakua kalamu, Mungu akamwongoza kuandika ule wimbo wa kuzindua.

Wote na wazisifie nguvu za Jina Lake Yesu!
Malaika na wamsujudie;
Ileteni taji ya kifalme,
Na mvikeni taji Bwana wa wote.

¹²⁰ Kipofu Fanny Crosby, wakati mmoja. Alisema, “Inamaanisha kitu gani kwako?” Baadhi... Yeye hakuuza haki zake za mzaliwa wa kwanza kama vile Mpentekoste Elvis Presley alivyofanya, ama kama Boone wa Kanisa la Kristo alivyofanya, ama kama Red Folley alivyofanya, wakiuza vipaji vyao kwa ulimwengu; walipata umati wa makadilaka, na dola milioni moja, santuri za dhahabu. Bali Fanny Crosby alidumu mwaminifu katika nafasi yake. Alipaza sauti:

Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
Sikia kilio changu kinyenyekevu;
Unapowaita wengine,
Usinipite.

Wewe ndiwe Kijito cha faraja yangu,
Wewe u zaidi ya uhai kwangu,
Nina nani duniani ukiacha Wewe?
Ama ni nani Mbinguni ila Wewe?

¹²¹ Wao walisema, “Vipi kama wewe ni kipofu utakapofika Mbinguni?”

Yeye akasema, “Nitamtambua, kwa vyovyote.”
Wakasema, “Utamjua?”
Kasema, “Nitamjua.”

Kasema, “Bibi Crosby, ungeweza kupata dola milioni moja.”

Kasema, “Sitaki hizo dola milioni moja.”

122 “Utamjua?” Yeye akasema:

Nitamjua, nitamjua,
Na nitasimama karibu Naye nikiisha
kukombolewa;
Nitamjua, nitamjua.

123 “Nisipoweza kumwona, nitahisi alama za misumari mikononi Mwake.” Akashinda lango la adui yake. Naam.

124 Kama uko ndani ya Kristo! Yeye alisema, “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu; ombeni ufunguo mnaotaka, ombeni lango mnalotaka kuteka; ombeni mtakalo, nanyi mtapewa. Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, mnaweza kuteka lango lolote la adui linalokuja mbele zenu.” Ninyi ni Uzao wa kifalme wa Ibrahimu.

125 Je! ni lango la aina gani linalosimama mbele yako? Kama ni ugonjwa, wewe ni zaidi ya mshindi kwake. Ndipo tunaweza kusema, tuimbe wimbo huu wa rehema wa kale:

Kila ahadi katika kile Kitabu ni yangu,
Kila mlango, kila kifungu . . . na ni cha Kiungu
sana,
Ninategemea upendo Wake wa Kiungu,
Kwa kuwa kila ahadi katika kile Kitabu ni
yangu.

126 Sisi ni zaidi ya mshindi, na uzao wa Ibrahimu utamiliki lango la adui! Wanaposema Mambo haya hayawezi kutukia, wanapotaka kuliita ni ibilisi, ama Beelzebuli, ama kitu fulani kingine, Mungu ni hakika atashinda kila lango na kumteka adui.

Na tuombe.

127 Bwana, jalia Uzao wa Ibrahimu. . . Ninajua wataliona, Bwana. Neno hilo linawezaje kuanguka bila ya kugusa hiyo Ardhi halisi? Ninaomba ya kwamba wao watafahamu sasa. Jalia kila mtu anayekuja kwenye mstari wa maombi aponywe.

128 Bwana, kukiwepo na wengine hapa ndani bado, ambao bado hawajakiri, hawajasimama hadharani na kumtetea Kristo, wakiwa tayari kukanusha kanuni zote za imani na vitu baridi, vya kidesturi, vilivyokufa ambavyo vimewaondoa Kwako. Na jalia wasimame sasa, na kusema, “Nitamkubali kama Mwokozi Wangu.” Ndipo basi utawatetea kwenye ile Siku.

129 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kama kuna wale ambao wangetaka kusimama kwa muda kidogo, kwa ajili ya maombi, waseme, “Ninataka kumtetea sasa, ili kwamba Yeye anitetea kwenye ile Siku, katika Uwepo Wake wa Kiungu.” Ninawaomba, na kuwapa fursa ili kwamba jina lako liandikwe kwenye Kitabu cha Uzima, endapo mtasimama. Siwaombi mjiunge na

kanisa lolote. Ninawaomba mje kwa Kristo, kama uko hapa na humjui Yeye.

¹³⁰ Mungu akubariki, mwanangu. Je! kuna mwingine, aseme, “Ni—ninataka kusimama sasa.” Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, dada yangu. “Ninataka...” Mungu akubariki. Mungu akubariki. “Ninaamua, alasiri ya leo.” Watu hawa wazuri, wanaume na wanawake, wanaosimama, “Nitaamua, alasiri ya leo.”

¹³¹ Na siku hiyo wakati daktari anaposema, “Vema, ajali ya barabarani; damu yake inamwagika, mauti iko juu ya mwanamume huyo ama mwanamke huyo.” Ama, asubuhi moja, utakumbuka msimamo wako. Wewe mtetee sasa.

¹³² “Kama ukinionea aibu mbele za watu, nitakuonea aibu mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu. Bali utanikiri mbele za watu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu.”

¹³³ Mungu akubariki, dada yangu. Je! kungekuwa na wengine roshani mahali fulani? Sasa hivi, wakati tuingojea. Baadhi yao, wengine zaidi kwenye ghorofa ya chini? Vema. Ninaamini neno lao, ewe mpendwa.

¹³⁴ Kama Neno likianguka kwenye Shamba lenye rotuba, kama maskini yule mwanamke kisimani, yeye—yeye alifahamu. Alikuwa amewakilishwa Mbinguni, tangu kuwekwa misi-... kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Wakati hiyo Nuru ilipoligusa, yeye alilitambua.

¹³⁵ Mungu akubariki, ndugu yangu. Huo ni ushujaa... Mungu akubariki, ndugu yangu. Huenda ulifanya mambo makuu maishani mwako; unafanya jambo lililo kuu sana ulilopata kufanya, sasa, mtetee Kristo.

¹³⁶ Baba yetu wa Mbinguni, mbegu imeanguka kwenye shamba fulani, alasiri ya leo. Tunaona Uhai ukiota. Wanaume na wanawake wanasimama kwa miguu yao, na jicho la Mungu linaloona kila mahali, Ambaye yupo mahali pote, anayejua yote, mwenye nguvu zote, anawaona hao. Hao ni wako, Baba. Ninawakabidhi Kwako sasa, kama tuzo.

¹³⁷ Jalia tukio hili lao la kusimama pale sasa, wakijua walivyofanya, wakijua maana ya jambo hili, ya kwamba wanasimama kuchukua msimamo wao na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Jalia wadumu waaminifu hata Siku watakayosimama katika Uwepo Wako, ndipo ile Sauti ya kupendeza itasema, “Naam, siku moja pale Baton Rouge, ama mji mdogo unaoitwa Denham Springs, yeye alinitetea, Baba, sasa Nami nitametea mwanamume huyo, ama mwanamke huyo.” Tujalie, Bwana. Hao ni Wako, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu awabariki, kwa ajili ya msimamo wenu. Mungu daima...

¹³⁸ Sasa nifanyieni jambo hili moja. Tafuteni, kama mko mahali hawa wachungaji walipo, waoneni wachache, zungumzeni nao. Endapo hamjabatizwa bado, katika ubatizo wa Kikristo, fanyeni hivyo. Ingieni miongoni mwa waamini sasa, waamini halisi, si wanaojifanya waamini; waamini halisi.

Wakati tukiomba, hebu na tuombe lesi hizi.

¹³⁹ Baba wa Mbinguni, lesi hizi zinaenda huko nje sasa; ambako, sikujui. Pengine baba fulani mzee anayeketi hapa nje kwenye bwawa dogo mahali fulani, akingojea lesi hii ije; maskini mtoto mchanga akilala pale kwenye kitanda cha hospitali; mama fulani anayesimama, akiugua kwa majonzi, akingojea kurudi kwa lesi. Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utaenda pamoja nazo. Na kwa ajili ya ishara ya Uwepo Wako leo, na imani yetu Kwako kama vile tulivyohubiri Neno Lako, jalia imani iliyokuwa ndani ya Ibrahimu, na imani iliyotolewa na tukapewa na Yesu Kristo, jalia iambatane na lesi hizi, na kumponya kila mtu atakayewekewa lesi hiyo. Tunazituma, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁴⁰ Sasa hebu kidogo tu, kabla hatujaitisha mstari wa maombi. Mungu mwenyezi na mwenye nguvu zote, Yule mkuu, Yeye ajitoshelezaye kwa yote...Tafadhalini, enyi wapendwa, ni—nitaanza kuwaombea wagonjwa, nami...Labda, tutakaposhuka, hu—huenda nisipate jambo lolote la kuwaambia; baadhi yenu huenda wakaondoka kabla ya wakati huo. Vyovyote ulivyo, hata kama hukusimama, muda mfupi uliopita, nawe huna hakika... .

¹⁴¹ Kama wewe ni mfuasi wa kanisa fulani, hilo ni jambo zuri, bali hilo si zuri vya kutosha. Unaona, yule mtawala kijana tajiri alikuwa ni mfuasi wa kanisa. Unaona? Alimwuliza Yesu angeweza kufanya nini ili apate Uzima wa Milele. Yeye kamwe hakuukubali. Aliondoka akaenda zake. Ni jambo la kijanga jinsi gani kufanya kwa yule kijana mwanamume. Usifanye alivyofanya. Je! unakumbuka mara ya mwisho alipozungumziwa? Baadaye kidogo, alifanikiwa. Akawa tajiri zaidi. Akafikia mahali ambapo hata maghala yake yalijaa yakafurika. Lakini baadaye tunapata habari zake za mwisho, kuzimu, miali ya moto ikimtesa. Usininii, usiache jambo hilo likupate. Mkubali Kristo.

¹⁴² Enyi vijana, enyi wasichana, wavulana, kwenye wakati pekee wa kubadilika kwa maisha, nawaomba mfanye hivyo. Nisikilizeni, kama—kama ndugu yenu, mtu anayewapenda. Niko hapa kwa sababu ninawapenda. Ninampenda Mungu, na ninawapenda, wala siwezi kumpenda Mungu kama siwapendi.

¹⁴³ Naona ni afadhali sana, kama mtu ulikuwa una tamshi la kutoa, litamke kwa mwanangu kule aliko, ama kwa mmojawapo wa watoto wangu. Hebu ni ninii tu...Mimi, nitakosa tamshi

hilo. Mzazi yeyote atafanya jambo hilo; vivyo hivyo na Mungu pia. Unaona? Kuwapenda watu Wake. Kupendana.

¹⁴⁴ Unasema, “Kwa nini unawakemea?” Upendo halisi husahihisha.

¹⁴⁵ Kama mtoto wako ameketi huko nje barabarani; unasema, “Vema, yule pale Kadogoo ameketi. Haimpasi kufanya hivyo, bali sitaki kuumiza hisi zake ndogo.” Humpendi. Atauawa huko. Kama unampenda, utamwingiza ndani na kumpiga kofi. Utamfanya atii.

¹⁴⁶ Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya. Upendo husahihisha, na huo ndio upendo halisi.

¹⁴⁷ Wakati mhubiri anaposimama na kuwaacha ninyi wanawake mkate nywele zenu, na kujipaka rangi na kadhalika, wala hawasahihishi, hakuna upendo halisi hapo; wala hatakemea jambo hilo. Na kukuacha wewe mwanamume uoe mara tatu ama nne, na mambo haya mengine yote, na kuwaachilia, hakuna upendo halisi hapo. Anawaacha mjiunge na kanisa, na kuwapapasa-papasa mgongoni, na kuwafunga kwa kanuni za imani, halafu, “Hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya, ni kujiunga na kanisa takatifu,” hakuna upendo hapo. Ama, aidha, mtu huyo amepotea kabisa, yeye mwenyewe, haoni.

¹⁴⁸ Upendo halisi husahihisha, na unakurudisha kwenye Neno la Mungu.

¹⁴⁹ Mwangelie Yesu, jinsi, yale aliyosema, maana Yeye aliwapenda, sana sana hivi kwamba alikufa badala yao, wakati ambapo hata walikuwa wakitaka kumwaga Damu Yake.

¹⁵⁰ Sasa naomba Roho Mtakatifu aliye mkuu...ninataka kungojea kwa dakika moja tu. Ninangojea mpaka upako wa Roho Mtakatifu utakaponijia, kabla hatujaanza. Nimekuwa nikihubiri. Asanteni, kwa ajili ya ushirikiano wenu.

¹⁵¹ Sasa, kila mmoja hapa ndani, popote ulipo, popote jengoni, omba kwa dakika moja tu, useme, “Bwana Yesu, nisaidie! Nisaidie! Nijalie niguse vazi Lako.” Yesu alisema, mwajua, wakati yule mwanamke alipogusa vazi Lake, Yeye hakuhisi jambo hilo, kimwili, bali aligeuka na kujua yeye alikuwa ni nani na kile alichofanya. Yeye ni Yesu yeye yule alasiri ya leo, Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana na mambo ya udhaifu wetu.

¹⁵² Je! mnaamini, kila mmoja wenu sasa, ya kwamba ni kweli, ya kwamba Mungu aliyetoa ahadi hii, mara nyingine tena (na jalia aonyeshe jambo hilo) ya kwamba tunaishi katika siku za Sodoma? Ni wangapi wanaoamini jambo hilo, humu jengoni, inua tu mkono wako.

¹⁵³ Tunaishi, tuseme, katika Sodoma. Mfumo wote mzima umechafuka, mfumo wa dunia, kila kitu, mfumo wa kanisa, mfumo wa kisiasa. Hakuna kitu. Siasa zimechafuliwa kabisa. Mifumo, kila mahali, watawala wetu wa mabavu, kila kitu ni

upotovu. Kanisa limekuwa vivyo hivyo. Familia zimekuwa vivyo hivyo. Ni upotovu tu, Sodoma!

154 Halafu, kumbuka, Mungu ameweka hilo mbele zako, basi kumbuka Yeye alisema ya kwamba angejiwakilisha Mwenyewe katika mwili wa kibinadamu, na angefanya kama alivyofanya kabla ya wakati wa Sodoma, kabla ya Mwana aliyeahidiwa kuja jukwaani. Yeye aliahidi kumtuma mtu ambaye angemtangulia huyo Mwana aliyeahidiwa, kama Yeye alivyofanya mara ya kwanza, ambaye angemtambulisha; Naye alisema, “Wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa.”

155 Mimi sikufahamu wewe. Vema, Bi Thompson, shida hiyo ya wanawake na matatizo chungu mbovu, je! unaamini kwamba Mungu atakuponya? Unaweza kuamini jambo hilo? Utaamini? Bi, Bi Thomas, unaamini atakuponya? Inua mikono yako, basi.

156 Kuna bibi mmoja anayeketi moja kwa moja nyuma yako. Anaomba. Ana yabisi kavu.

157 Mtu aliyeketi karibu naye, ana shida ya tumbo, naye pia anaomba. Utaukosa, usipokuwa mwangalifu. Hutoki hapa. Unatoka Mississippi. Wewe ni Bw. na Bi. Kramer. Kama unaamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakuponya. Kama unaweza kuamini. Unaamini? Basi unaweza kuupokea. Sawa. Inueni mikono yenu kusudi watu wapate kuona ya kwamba ndio ninyi.

158 Siwajui watu hao. Sijapata kuwaona, maishani mwangu. Unapaswa kuamini, ewe mpendwa. Yeye anajitambulisha Mwenyewe. Je! mnaamini jambo hilo, kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

159 Kwa nini ulitikisa kichwa chako, bwana, na kuniangalia namna hiyo? Naam, bwana. Kwa sababu umefanya hivyo, nitazungumza na wewe kwa dakika moja. Wewe kwa namna fulani u mzee mwungwana unayeketi papa hapa, ukiniangalia. Yeye aliniangalia, kwa uaminifu sana. Aliamini jambo hilo. Unamwombea mtu fulani aliyekuwa na kiharusi. Lakini—lakini jambo muhimu unaloombea, unahitaji, unatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. A-ha. Hiyo ni kweli. Kama unaamini jambo hilo! Bibi huyo, unatafuta kazi ya kuajiriwa. Mbali na jambo hilo, kusudi upate kujua kwamba mimi ni nabii wa Mungu, ama mtumishi, umekuwa na upasuaji mara mbili. Umekuacha kidogo umedhoofika. Kila namna ya maradhi, tatizo la kiroho. Ninataka kukwambia zote zimetatuliwa. Imani yako inakuponya.

160 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...anayeketi karibu kabisa na wewe pale. Yeye anaomba. Angalia hapa. Yeye alikusikia, nawe umemgusa. Sikujui mimi, bali Yeye anakujua. Nitakwambia ulichokuwa ukiombea. Je! unaamini kwa moyo wako wote? Una ugonjwa wa kibofu nyongo, unaomba. Je!

unaamini ya kwamba Mungu atakuponya na kukufanya mzima? Wewe ni Bibi Smith. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako.

¹⁶¹ Unaona, Yeye anajitambulisha Mwenyewe. Ni kitu gani? Ni Uzao wa Ibrahimu, imani ambayo Ibrahimu alikuwa nayo, Bwana Yesu Kristo miongoni mwetu, akithibitisha Neno Lake, pamoja na ishara zinazofuata.

¹⁶² Ni nani, ni kadi ngapi zitakazoombewa, inueni mikono yenu, je! mna kadi zenu? Loo, afadhali tuanzishe mistari wa maombi.

¹⁶³ Mnaona, mnaelewa sivyo? Sasa huyo roho si kwamba tu... Hilo haliponyi. Hilo linamtambulisha tu kwamba Yeye yupo hapa. Wachungaji wenu wana mamlaka yale yale kuwaombea wagonjwa. Hawafanyi hivyo; la, la hasha. Lakini wao—wana mamlaka yale yale, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

¹⁶⁴ Sasa nawataka marafiki zangu wachungaji hapa. [Ndugu Branham anamwuliza mtu fulani, “Je! ni sawa kuwaita kutoka kwa wasikilizaji, enyi wahudumu?”—Mh.]

¹⁶⁵ Ni wachungaji wangapi hapa wanaoamini kwa moyo wenu wote, wahudumu walio hapa ndani, wanaoamini? Loo, asanteni. Sijui kama mtasimama? Njoni hapa, simameni pamoja na mimi kwa dakika moja tu, papa hapa chini, muwaombea wagonjwa. Shukeni mje moja kwa moja hapa. Sasa angalieni uponyaji ukitukia, angalieni kile kinachotukia.

¹⁶⁶ Ninawatakeni mje, mfanye mistari mi—miwili papa hapa. Ninashuka kuja hapo chini mara moja tu, kuwaombea wagonjwa. Ninataka wachungaji wanaoamini wanaotaka kujitambulisha kama waaminio. Kwamba, mnaamini, kwamba kuja kwenu hapa, mnaishi maisha matakatifu, masafi. Kumbukeni, angalieni hapa kile kinachotokea, kikiiwakilisha Injili ya Kristo!

¹⁶⁷ Ndugu Blair, ninakujua wewe pale, wewe ama Ndugu Pat. Je! mnaweza kuipanga mistari hiyo miwili jinsi mnavyofanya kwa kawaida, nawaomba, wewe na Ndugu Pat.

¹⁶⁸ Wachungaji waamini watakaoamini! Sasa, angalia, kama Mungu anaweza kujitambulisha jinsi hiyo kwa Neno Lake, pamoja na Neno Lake, je! ni wangapi wanaojua ya kwamba Biblia, Yesu alisema hivi, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya”? Wachungaji, mmekuja hapa kujitambulisha kama waaminio. Ninyi ni waaminio? Ninyi ni waaminio (sivyo?), msingekuwa mmesimama hapa. Sasa Yesu alisema nini? “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Mimi ni mwamini pamoja na ninyi.

¹⁶⁹ Ninashuka kuja huko. Hawa ni watu wetu, nasi ni wachungaji juu ya makundi haya. Ninashuka kuja kutandaza nyavu zangu pamoja na zenu sasa, kuweka mikono yangu pamoja na yenu. Na wakati watu hawa wanapopita, kama

una kitu chochote ambacho kinashuku tu kidogo niani mwako, kiondoe sasa hivi; ili kwamba watu hawa watakapopitia hapa, basi kila mmoja wao akipita, nasi tuweke mikono yetu juu yao, wataponywa. Je! mtaamini kwa moyo wenu wote sasa, kila mtu? [Wahudumu wanasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁷⁰ Ni wangapi hapa ndani watakaowaombea wengine wanapopita, inua mkono wako, “Nitakuwa nikiomba.”

¹⁷¹ Kumbuka, huenda ikawa ni baba yako, mama yako, binti yako ama mwanao, dada ama ndugu. Na kama si wako, ni wa mtu fulani, ambaye atapitia kwenye mstari huu. Na vipi kama ilikuwa ni wao, nao walikuwa wakifa kwa kansa, ama ugonjwa fulani wa kutisha, hivi usingetaka mtu awe mwaminifu sana? Hakika, tungetaka.

¹⁷² Sasa, ninaamini, utaninii vipi. . . Sasa hawa walio kwenye safu *hii* hapa, marefu haya ya kanisa, simameni mkiegemea upande *ule*, mkiwa na kadi ya maombi. Simameni mkiegemea upande *ule*, wote mlio kwenye sehemu ya kulia. Sasa, jinsi ambavyo, shikilieni sehemu ya kushoto; tunasongamana sana, mnaona, wala hamjui ni jinsi gani, vile tunavyofanya. Vema, wote walio kwenye sehemu *hii*, simameni *hapa*. Sasa, wote walio kwenye sehemu ya mkono wa kulia, njoni tu upande huu, maana mtashuka mje huku, zungukeni.

¹⁷³ Na mtaendaje, watatokaje, Ndugu Borders? Moja kwa moja kupitia kwenye mlango wa kando, wazunguke moja kwa moja kisha waingie jengoni tena.

¹⁷⁴ Kwa hiyo, wakati upande *huu* utakapoitwa, katika dakika chache, nao watasimama. Na hebu tuone sasa vile. . . Vema, hao walio kwenye sehemu *hii*, geukeni upande huu hapa. Shikeni kadi zenu za maombi, njoni upande huu. Na ninyi mlio kwenye roshani, shukeni mje moja kwa moja mkakutane nao mwishoni mwa safu hiyo hapo juu. Sasa hawa walio kwenye sehemu ya mkono wa kushoto, nendeni kuelekea sehemu ya mkono wa kushoto. Halafu basi, mnaona, ninyi mfanye mstari wenu na mrudi nyuma kuelekea upande *ule*; mgeuke mrudi, mgeuke namna *hiyo*. Mnaona? Nanyi mtaufuata mstari huo moja kwa moja mkizunguka, ndipo basi hatutakuwa na mchanganyiko wowote hata kidogo.

¹⁷⁵ Halafu basi ninyi mlio kwenye roshani, chukueni nafasi zenu moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa, na mwingie moja kwa moja wakati wakipita.

¹⁷⁶ Sasa, sasa anzeni tu kutembea kurudi nyuma, kila mmoja, rudini moja kwa moja nyuma mpaka mtakapokutana na mstari huu moja kwa moja kuzunguka *hapa*. Zungukeni moja kwa moja, *hapa* juu, anzeni tu kuzunguka moja kwa moja na mje kwenye mstari huu papa *hapa*.

177 Loo, ni kitu gani kingeweza kutukia sasa hivi! Ni kitu gani kingeweza kutukia! Huu utakuwa ni wakati ambapo jambo fulani halina budi kutukia. Vema.

178 Sasa, hiyo ni kweli, rudini moja kwa moja kuzunguka upande *ule*, na mwingie moja kwa moja mstarini, namna hiyo. Zungukeni moja kwa moja kwenye marefu haya ya kanisa. Hiyo ndiyo njia sasa.

179 Na sasa wakati mnaposimama, kila mtu kwa miguu yake, tutaomba maombi. Na kusanyiko hili litaomba pamoja na mimi, ya kwamba mtaponywa. Iweni tu na imani sasa. Wala msininii. . .

180 Njoni moja kwa moja huku, huko nyuma kabisa, zungukeni moja kwa moja mkajiunge na mstari huu huku nyuma. Zungukeni moja kwa moja, mpange mstari mmoja mkubwa. Zungukeni moja kwa moja upande *ule*, na mfanye mstari mmoja. Naam.

181 Kila mtu awe katika maombi. Iweni kweli katika imani sasa. Sasa msiuangalie kabisa umati sasa. Kumbukeni, tumeninii—tumefunikwa na Uwepo wa Yesu Kristo, akitutegemea kuheshimu yale aliyofanya miongoni mwetu, kwa kuwa na imani katika Neno Lake.

182 Hilo ni sawa. Sasa itakuwa tu ni sawa. Nafikiri mstari huo unaingia vizuri sana.

183 Sasa wakati wote wamesimama, ninataka kila mtu sasa, humu jengoni, uinamishe kichwa chako.

184 Bwana Yesu, litatukia hivi karibuni. Uamuzi unapaswa kufanywa sasa hivi. Je! sisi tunaamini ya kwamba Wewe upo hapa? Je! tunakupenda? Je! tuna imani, Bwana, ya kutosha kwa yale tutakayoomba? Watu hawa wanajitambulisha kwa kusimama kwenye mstari *ule*. Bwana, jalia isiwe ni bure. Jalia iwe, Bwana, kwamba watapitia hapa, kila mmoja atapita tu kana kwamba walikuwa wakipitia chini ya Kristo, kwa kuwa tunajua Yeye yupo hapa. Na tunaomba ya kwamba wao watapokea uponyaji wao. Nina hakika ya kwamba hata baada ya majuma na majuma yajayo, watu hawa watakuwa wakienda kwa wachungaji wao, wanawake waliokuwa na ugonjwa wa akina mama, kuumwa na tumbo, wanaume wenye unyong'onyevu, maradhi ya kila namna, wataponywa, wakisema, "Unajua, kitu hicho kiliniacha sasa hivi," kwa kuwa wao wako Uweponi Mwako. Jalia wapite sasa na—na wachukue hili ambalo wewe umelifia. Wao ni Uzao wa Ibrahimu, Nawe umewashindia. Jalia waje wapokee kile ambacho umewapa.

185 Na, Shetani, umekwisha kuwekwa wazi sana juma hili, mpaka unajua ya kwamba wewe ni kiumbe kilichoshindwa. Yesu Kristo alikushinda pale Kalvari. Alifufuka siku ya tatu, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, Naye anasimama kati yetu sasa. Na imani yetu inamwangelia Yeye, na tunakupaa kisogo au kukipaa

kisogo chochote kile ulichofanya. Waache hawa watu, katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁸⁶ Vema, anza mstari. [Ndugu Branham pamoja na wahudumu wanaawawekea wagonjwa mikono na kumwombea kila mtu kwenye mstari wa maombi. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁸⁷ Tumefanya tu jinsi ambavyo Bwana ametuagiza kufanya. Ni wangapi wenu waliopitia kwenye mstari huo, walioamini ya kwamba mtakuwa wazima, inua mkono wako. Ninaunganisha wangu pamoja nanyi.

¹⁸⁸ Tulichokuwa tukifanya pale, hatimaye, kama kundi la wahudumu pale; wengi wao walikuwa wagonjwa, nilijua jambo hilo, ila wanajaribu kujitahidi kusudi wapate kuliingiza kusanyiko lao, kama wataingia ama hawataingia. Hao ni wachungaji halisi. Na Roho Mtakatifu aliniambia, “Wafanye washikane mikono wao kwa wao.” Tuliunganisha mioyo yetu na nyavu zetu pamoja, na maombi yetu, pamoja.

¹⁸⁹ Yesu, waponye, pia. Na uwafanye wachungaji wenye nguvu, wenye nguvu katika Neno la Bwana.

¹⁹⁰ Naomba Mungu, ndugu zangu, awape shauku zote za moyo wenu. Naomba mumtumikie siku zote, na mwe na nguvu za Mungu maishani mwenu, mpate kuhudumia kundi hili zuri la watu. Naomba Yesu Kristo, ambaye amekuwa pamoja nasi, na yuko pamoja nanyi wakati wote, na ajitukuze kwenu kuliko vile amewahi kufanya hapo nyuma.

¹⁹¹ Enyi watu, baadhi yenu ambao mlikuwa mmelemaa, huenda msione tofauti kwa kitambo kidogo, huenda msione tofauti. Angalieni vile Ibrahimu alivyofanya. Haileti tofauti yoyote kwamba ni nini; hilo silo unaloangalia. Huangalii dalili zako. Angalia kile Yeye alichosema. Kama ukisema, “Ningali ninasikia maumivu,” hilo halina uhusiano wowote na jambo hilo. Umefanya yale Mungu aliyosema ufanye. Unaona, usiangelie hilo. Angalia yale aliyosema. Mungu alisema ilikuwa hivyo! Ninaamini. Na ninyi je! [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kwa moyo wangu wote, ninaamini.

¹⁹² Bwana Mungu awabariki mpaka nitakapowaona tena. Maombi yangu ni kwa ajili yenu; usiku hauwi na giza mno, mvua hainyeshi mno. Nitakuwa nikiwaombea. Ninyi niombeeni. Mpaka tutakapoonana tena, Mungu awabariki. Sasa ndugu anayehudumu, mnaona.



KUMILIKI LANGO LA ADUI BAADA YA KUJARIBIWA SWA64-0322

(Possessing The Gate Of The Enemy After Trial)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 22 Machi, 1964, kwenye Shule ya Sekondari ya Denham Springs huko Denham Springs, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2008 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org